JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM

**MASHTAKA YA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA MITANDAONI), 2018**

**SHAURI NA. 08 - 2018/2019**

**FELIX RED**

# UAMUZI

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA YA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA MITANDAONI), 2018.**

## 1.0 Utangulizi

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa leseni ya kutoa maudhui mtandaoni kwa **FELIX RED**, kwa ajili ya kuchapisha na kutangaza habari mbali mbali mitandaoni.

1.2 Kwa mujibu wa Kanuni ya 4 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu la kutunza kumbukumbu za watoa huduma wote wa maudhui mtandaoni pamoja na

kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mtoa huduma yoyote wa maudhui mitandaoni atakayekiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni au sheria nyingine.

1.3 Mtoa huduma wa maudhui mtandaoni, **FELIX RED** anatuhumiwa kukiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni, ambapo mnamo tarehe 05 Mei, 2019 aliweka maudhui yenye lugha ya matusi kupitia chaneli yake iliyoko katika mtandao wa Youtube. Maudhui hayo yalirushwa kwa picha jongefu kwa kunakili chapisho la mtandao wa kijamii wa Instagram wa **Bi. *Rachel A. Temu*** lenye kichwa cha habari ***"tempestitiously."*** **Bi. Rachel A. Temu** alisimulia mambo yanayohusu msiba wa Dkt. Reginald Abraham Mengi kwa kutoa lugha ya matusi na yenye kuwadhalilisha na kuwasononesha waombolezaji na jamii kwa ujumla.

1.4 Maudhui hayo yalitangazwa bila ya kuzingatia weledi ambapo **FELIX RED** iliweka picha ya marehemu Dkt. Mengi na mke wake na kuweka picha jongefu ya **Bi. Rachel A. Temu** aliyetoa matusi hayo ya nguoni.

1.5 Katika picha jongefu hiyo, **Bi. *Rachel A. Temu*** alisikika akizungumza maneno yafuatayo; ***"...lazima mvae kama mnaenda Hollywood, ule ni msiba mkubwa, kuna Mabalozi, yaani pale kudanga full time....mmojawapo ni yule kahaba wa Paris ambaye alikuwa anakula na babu, kuna Kuma vibuyu kama hawa ambao wameingia wanatafuta mabwana halafu hawajulikani, kwa hiyo kama ulikuja hapa na mkundu wako kudanga unatafuta bwana pole yako Kuma kibuyu...sijui unaitwa Winnie Lips, wewe unaitwa Winnie Lips Kuma la mama yako au unaitwa Winnie sura kama kuma ya Amber Rutty.. kwa sababu shoga yako umejishongodoa kujisemesha semesha ndugu yangu hujulikani...".***

1.6 Kwa kuweka picha jongefu hiyo, **FELIX RED** imekiuka/imevunja Kanuni Namba 5(1) (a); (b); 5 (2) (b); 12(a); (b); (h) na (f) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni) 2018, ambazo zinasomeka kama ifuatavyo;

*5(1) For the purpose of these Regulations, an online content provider shall have the obligations to;*

*(a) ensure that online content is safe, secure and does not contravene the provisions of any written law;*

*(b) take into account trends and cultural sensitivities of the general public.*

*5(2) A subscriber and user of online content services shall;*

*(b) ensure his posts do not contravene the provisions of these Regulations and any other written law.*

*12 Online content services provider shall not publish;*

*(a) indecent content save for sex and nudity sex scenes approved by the body responsible for film censorship;*
*(b) Obscene content;*
*(h) Content that causes annoyance, threatens harm or evil, encourages or incites crime, or leads to public disorder;*
*(f) content that portrays violence, whether physical, verbal or psychological; that can upset alarm and offend viewers and cause undue fear among the audience or encourage imitation;*

**2.0 Wito wa kufika mbele ya Kamati ya Maudhui.**

2.1 Mnamo tarehe 22 Mei, 2019, Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa **FELIX RED** wito wa kufika mbele ya Kamati kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

2.2 Tarehe 31 Mei, 2019, saa 04:00 Asubuhi, uongozi wa **FELIX RED** ukiongozwa na Bw. **Felix Justine Kawishe** ulifika mbele ya Kamati ya Maudhui kwa ajili ya kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

## 3.0 Kusikiliza na Kuangalia Maudhui Mtandaoni ya FELIX RED ya tarehe 5 Mei, 2019

Kamati ya Maudhui na Uongozi wa **FELIX RED** walisikiliza na kuangalia maudhui mtandaoni ya tarehe 05 Mei, 2019 yaliyochapishwa na **FELIX RED** katika chaneli yake ya Youtube ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni.

## 4.0 Maelezo ya Utetezi ya FELLX RED.

Uongozi wa **FELIX RED** uliwasilisha utetezi wake kwa Kamati na imekiri kosa walilolifanya na kuomba radhi kwa kukiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni kwa kuchapisha maudhui yenye lugha ya matusi katika mtandao wao wa Youtube mnamo tarehe 5 Mei, 2019.

**FELIX RED** imeendelea kuahidi kuhakikisha kuwa itafuatilia kwa makini kila maudhui kabla ya kuyaweka mtandaoni ili kuhakikisha kuwa tatizo kama hili halijitokezi tena.

5.0 **Felix Justine Kawishe** ambaye ni Msimamizii na Muendeshaji wa **FELIX RED** alianza kwa kukiri kwamba, kutokana na uzembe wake, wa kutokukagua maudhui yaliyokua kwenye video hio,aliiweka kwenye mtandao wake na hivo kupelekea maudhui hayo mabaya yenye kukera na kuharibu jamii kufika kwa hadhira (jamii) na kisha kuomba msamaha kwa kuchapisha mtandaoni maudhui yenye matusi. Alidai kwamba chaneli yao ni changa na alikuwa akiiendesha pekeyake japokuwa kwa sasa amepata wenzie wawili wa kumsaidia.

Alisema kuwa ameshayaondoa maudhui hayo mtandaoni tangu tarehe 29 Mei, 2019 baada ya kupigiwa simu na TCRA.

## 6.0 Majumuisho ya Utetezi wa FELIX RED.

Katika kujumuisha utetezi wao, **Felix Justine Kawishe** alizidi kuomba radhi na kusema kuwa **FELIX RED** ni mara ya kwanza kutenda kosa hilo na kuahidi kuwa

Mwandishi wa habari ambaye atakuwa anamsaidia kaitika kuendesha shuguli mbalimbali za mtandao huo.

Pia **FELIX RED** iliahidi kuwa balozi mzuri wa Kamati katika kuelimisha jamii juu ya matumizi sahihi ya vyombo vya maudhui mtandanoni na kwa sasa atajikita Zaidi katika kutoa maudhui yanayelimisha jamii tu.

## 7.0 Tathmini ya Kamati

7.1 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba **FELIX RED** imefanya kosa la kuchapisha maudhui yenye matusi mtandaoni kwa uzembe kwani ilitakiwa kuwa makini na kuzingatia na kufuata Sheria, Kanuni na maadili ya Utangazaji.

7.2 Kamati ya Maudhui imebaini kuwa utetezi wa **FELIX RED** hauna msingi na kwamba maudhui aliyochapisha hayakuzingatia weledi.

## 8.0 Ushauri wa Kamati kwa FELIX RED

8.1 Kamati inalengo la kuimarisha tasnia ya habari na utangazaji na kuwa haina nia ya kubana ubunifu wa watangazaji, bali inawataka wanahabari kuzingatia weledi Sheria na Kanuni na maadili.

Hata hivyo kutokana na kosa lililobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa **FELIX RED** kuweka usimamizi wa matangazo ili kuhakiki maudhui yao ni salama kisheria kabla ya kuwekwa mtandaoni. Hatua hiyo itaiwezesha **FELIX RED** kuepuka kuvunja sheria na Kanuni za nchi.

## 9.0 Uamuzi wa Kamati

9.1 Baada ya kusikiliza na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi yaliyotolewa na Uongozi wa **FELIX RED**, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa **FELIX RED** kupitia chaneli yake katika mtandao wa kijamii wa Youtube imekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mitandaoni), 2018.

**HIVYO BASI**, Kamati ya Maudhui imeamua yafuatayo:

**FELIX RED** Kulipa faini ya **Shilingi Milioni Tano (TZS. 5,000,000.00)** tu kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa mujibu wa Kanuni Na. 18 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mitandaoni), 2018;

Pamoja na faini hiyo **FELIX RED** inapewa Onyo Kali na, pia inaamriwa kuomba radhi kwa Watanzania kwa kosa lililofanyika kupitia chaneli yao ya Youtube kwa siku saba (7) mfululizo kuanzia tarehe 05/06/2019;

Uamuzi huu umetolewa na kusomwa Dar es Salaam leo tarehe **04** mwezi **Juni** mwaka **2019**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia leo.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Bi Valerie Ndeneingo-Sia Msoka**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

........................................................

**Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

**PAMOJA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Bwana Joseph Method Mapunda** ........................................
2. **Bwana Abdul Ramadhani Ngarawa** ........................................
3. **Bwana Derek Kaitira Murusuri** ........................................
4. **Bwana Jacob Gregory Tesha**